



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZAMITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO



TANGAZO LA KAZI ZA UFUNDI

NAMBA: LGA/005/2020/2021/CHUO/W/ 1 LOT 1- 16

KWA AJILI YA KAZI YA UJENZI CHUO CHA UALIMU NGORONGORO

TAREHE 14, DISEMBA, 2020

Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro imepokea fedha kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ualimu. Fedha hizi zitatumika katika ujenzi wa majengo na miundo mbinu ya Chuo cha Ualimu Ngorongoro. Njia ya ununuzi itakayo tumika wakati wa Ujenzi ni Force Account kwa kuzingatia maelekezo ya matumizi ya njia kwa mujibu wa Kanuni Na.167 ya ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016. Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Ngorongoro chini ya Sheria ya manunuzi ya umma Na.7 ya mwaka 2011 kanuni Na.181 anawatangazia wananchi, makampuni na taasisi mbalimbali kuomba kazi za ufundi (local fundis) katika ujenzi wa Chuo kipya cha Ualimu Ngorongoro, ambapo majengo yatayo jengwa ni kama ifuatavyo:-

1. LOT 1 UJENZI WA JENGO LA UTAWALA
2. LOT 2. UJENZI WA BLOCK MOJA YA MADARASA MATATU
3. LOT 3. UJENZI WA BLOCK MOJA YA MADARASA MATATU
4. LOT 4. UJENZI WA BWENI LA WASICHANA NA KICHOMEA TAKA
5. LOT 5. UJENZI WA BWENI LA WAVULANA
6. LOT 6. UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI (TWO IN ONE)

Kny: MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO

7. LOT 7. UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI (TWO IN ONE)
8. LOT 8. UJENZI WA NYUMBA YA MKUU WA CHUO MOJA
9. LOT 9. UJENZI WA MAABARA YA BIOLOJIA NA KEMIA
10. LOT 10. UJENZI WA MAKTABA NA CHUMBA CHA COMPUTA
11. LOT 11. UJENZI WA VYOO VYA WANAFUNZI MATUNDU 20
12. LOT 12: UJENZI WA BWALO NA JIKO LA CHAKULA
13. LOT 13: KAZI YA UFYATUAJI WA TOFALI
14. LOT 14. KAZI YA UWEKAJI WA TARAZO
15. LOT 15. KAZI YA PLUMBING KATIKA MAJENGO HAPO JUU
16. LOT 16. KAZI YA KUWEKA UMEME KWENYE MAJENGO HAPO

MASHARTI MUHIMU YA ZABUNI/MWOMBAJI

- i. Awe Raia wa Tanzania
- ii. Waombaji wawe wamesajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
- iii. Awe na cheti cha ufundi wa kazi husika kutoka VETA au taasisi nyingine zinazotambuliwa na Serikali au awe na uzoefu wa zaidi ya miaka mitatu kwa kufanya kazi katika taasisi za Serikali
- iv. Mwombaji awe na uwezo au uzoefu wa kusoma na kutafsiri michoro/ramani mbalimbali za ujenzi na utambuzi wa aina mbalimbali za vifaa vya ujenzi
- v. Muombaji aambatanishe uthibitisho wa uzoefu aliyonao
- vi. Muombaji aoneshe bei ya kujenga jengo husika kwa kila hatua.
- vii. Muombaji haruhusiwi kuomba jengo zaidi ya moja
- viii. Awe na mtaji wa kutosha kwa maana ya rasilimali Fedha, watu na vitendea kazi muhimu
- ix. Mwombaji aoneshe mawasiliano sahihi ikiwemo namba za simu, barua pepe au anwani za makazi yakiwa yamepitshwa na kugongwa mhuri wa Mtendaji wa Kata anakotoka
- x. Mwombaji ahakikishe fomu ya dhamana ya zabuni imejazwa kwa uhakika bila kukosewa
- xi. Mwombaji ahakikishe fomu zote za maombi ya zabuni zimejazwa kwa uhakika bila kukosewa
- xii. Maombi ya barua yaambatane na risiti ya malipo za maombi ya kitabu cha zabuni Tshs 50,000/=kwa kila ombi la zabuni, kupitia

Kny: MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO

Control namba inayopatikana katika ofisi ya Mweka Hazina wa Halmashauri (Mawasiliano 0784598490/0767568394)


- xiii. Maombi yanatakiwa kutumwa kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri na kuonyesha aina ya zabuni inayo ombwa bila kuwa na viashiria vyovyote na mahali inakotoka na yatumwe kwa anuani ifutayo;

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO,
SLP 1,
LOLIONDO.**

NB. Ramani/mchoro na nyaraka za zabuni zinapatikana katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.

Muda na Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21/12/2020 saa 5.00 asubuhi na zabuni zitafunguliwa saa 5.30 asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Waombaji au Wawakilishi wanatakiwa kuhudhuria kwenye ufunguzi


**ELINLAA M. KIVAYA
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NGORONGORO.**



Nakala:

Mbao za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro
Mkurugenzi Mtendaji Jiji la Arusha
Wakurugenzi watendaji Halmashauri za Wilaya ya
(Arusha, Meru, Monduli, Karatu na Longido)

Mbao za matangazo katika kata zote za Wilaya ya Ngorongoro na Wilaya za karibu.